PDPC FARAGHA NEWSLETTER

Toleo Na. 0007 Julai - Septemba 2026

PDPC na OUT Wazindua Programu Maalum ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi Waliothibitishwa (CDPOP).

"Ushirikiano wa PDPC na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) ni msingi imara wa kujenga wataalamu wenye weledi wa kweli katika fani ya ulinzi wa taarifa binafsi. Mafunzo haya yapo kisheria na ni lazima kwa kila DPO aliyeteuliwa kuyapata ili kuhakikisha anatekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kikamilifu," alisema **Dkt. Mkilia.**









YALIYOMO

03 PDPC na OUT Wazindua Programu Maalum ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi Waliothibitishwa (CDPOP).

06 PDPC Yaanza Ukaguzi kwa Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi Nchini.

08 Jamii Yaaswa Kuwa Makini Inapoweka Taarifa Binafsi Mtandaoni.

09 Habari Picha.

12 Makala Maalum.

15 Taarifa kwa Umma.

17 Matangazo.

18 PDPC Yawatahadharisha Wakulima Usalama Wa Taarifa Binafsi Kidigitali.



PDPC na OUT Wazindua Programu Maalum ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi Waliothibitishwa (CDPOP).

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) tarehe 13, Julai 2026 wamezindua rasmi Programu ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) Waliothibitishwa (Certified Data Protection Officers Program).

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia amesema licha ya taasisi nyingi kutekeleza takwa la kuteua DPOs imebainika kuwa maafisa hao wana taaluma na viwango tofauti vya uelewa wa dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi.

"Ushirikiano wa PDPC na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ni msingi imara wa kujenga wataalamu wenye weledi wa kweli katika fani ya ulinzi wa taarifa binafsi. Mafunzo haya yapo kisheria na ni lazima kwa kila DPO aliyeteuliwa kuyapata ili kuhakikisha anatekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kikamilifu," alisema Dkt. Mkilia.

"Nitoe rai kwa viongozi wa taasisi zote Nchini kuwawezesha Ma-DPOs wenu kushiriki programu hii. Hii ndiyo njia ya kuimarisha utawala bora na kujenga imani ya wananchi katika huduma mnazozitoa," alisisitiza Dkt. Mkilia.

Wakati huo huo Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Prof. Alex Makulilo, amesema kuwa programu hii si semina ya kawaida, bali ni mafunzo mahususi ya kina yatakayofundishwa kwa nadharia na vitendo.


“Awamu ya kwanza ya Programu hiyo inaanza rasmi tarehe 10 Agosti, 2026 na itakuwa na moduli tano, itafundishwa kwa muda wa siku 14 na itagharimu Tsh. 2,500,000 kwa kila mshiriki na mwisho wa mafunzo hayo, washiriki watafanyiwa tathmini ya kina na kisha kuthibitishwa na PDPC” alisema Profesa Makulilo.

Dhamira kuu ya Tume ni kuona Tanzania inakuwa na Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi wenye ujuzi, weledi na umahiri mkubwa wa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata kikamilifu matakwa ya sheria ya kulinda faragha za watu.





Baadhi ya watumishi wa PDPC na OUT wakisikiliza kwa Makini hutoba zilizokuwa zinatolewa na viongozi wa Taasisi hizo wakati wa hafla fupi ya Uzinduzi rasmi Programu ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi Waliothibitishwa (Certified Data Protection Officers Program), iliyofanyika katika viwanja vya makao makuu ya OUT jijini Dae es Salaam, tarehe 13, Julai 2026.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akizungumza na Waandishi wa Habari (Hawapo pichani) kwenye Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika Agosti 28, 2026 jijini Dodoma.

PDPC Yaanza Ukaguzi kwa Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi Nchini

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imeanza zoezi la ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) kwa kutembelea taasisi, mashirika na wafanyabiashara wanaokusanya na kuchakata Taarifa Binafsi Nchini.

Hayo yameelezwa Agosti 28, 2026 jijini Dodoma na Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia wakati akizungumza na vyombo vya habari ambapo amesema ukaguzi huo wa kutembelea taasisi, mashirika na wafanyabiashara mbalimbali Nchini unalenga kujiridhisha iwapo wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi wanazingatia matakwa ya Sheria katika shughuli zao.

Miongoni mwa mambo yanayokaguliwa ni usajili wa taasisi katika rejesta ya Tume, utekelezaji wa majukumu ya Afisa Ulinzi wa Taarifa (DPO) katika taasisi husika, pamoja na namna Taarifa Binafsi zinavyokusanywa, kuchakatwa na kuhifadhiwa ili kuhakikisha taratibu zilizowekwa kisheria zinafuatwa.

Eneo jingine litakalokaguliwa ni utaratibu unaotumika kusafirisha Taarifa Binafsi nje ya Nchi, kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa chini ya Vifungu vya 31 na 32 vya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA).

Aidha, PDPC imeeleza kuwa itachunguza hatua zinazochukuliwa na taasisi katika kulinda Taarifa Binafsi dhidi ya upotevu, uteketezaji, ubadilishaji au kuchakatwa bila idhini, kama inavyoelekezwa katika Kifungu cha 27(1) cha Sheria hiyo.

Ukaguzi huo ni moja ya majukumu ya Tume, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya taasisi,



mashirika au wafanyabiashara watakaobainika kutokidhi matakwa ya Sheria, ikiwamo kutolewa kwa adhabu na faini kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.







Jamii Yaaswa Kuwa Makini;
Inapoweka Taarifa Binafsi Mtandaoni

Jamii yashauriwa kuzingatia ulinzi wa Taarifa zao Binafsi pindi wanapotaka kuziweka kwenye Mitandao ya Kijamii.

Akizungumza katika mahojiano maalumu kupitia kipindi cha Kumepambazuka kilichorushwa hewani na Redio one Agosti 27, 2026, Afisa Habari Mwandamizi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Bi. Joseline Chambasi ametoa wito kwa wananchi kuwa makini na Taarifa Binafsi wanazoziweka kwenye mitandao ya kijamii.

"Wito ninaotoa kwa watanzania ni kuhakikisha wanalinda Taarifa zao Binafsi kwakua zikitumika vibaya zinaweza kuleta madhara kwao au hata kwa familia zao. Hivyo kikubwa, kama si lazima usiweke Taarifa zako binafsi kwenye mitandao ya kijamii kwasababu hujui nani atakutana nazo na atazitumiaje." Amesema Bi. Chambasi.

Aidha Bi. Chambasi aliendelea kuwataka wananchi kutokuogopa kutoa Taarifa zao ili kupata huduma kwenye taasisi au ofisi mbalimbali nchini, bali wahakikishe wanatoa Taarifa zao na kupatiwa huduma kwenye Taasisi iliyosajiliwa na kupata vyeti husika kutoka PDPC.

"Mtu asiogope kupata huduma kwenye Taasisi yoyote Nchini, bali ahakikishe amejiridhisha kuwa Taasisi hiyo imesajiliwa na ina vyeti halali kutoka PDPC" alisema Bi. Chambasi

Katika hatua nyingine Bi. Chambasi alitamatisha mahojiano hayo kwa kuzijulisha Taasisi na Ofisi zote nchini kwamba Kujisajili PDPC sio hiyari bali ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA).





HABARI PICHA

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Mhe. Balozi Adadi Rajabu akiongoza Kikao cha Kumi cha Bodi hiyo ambacho kimepokea na kujadili utendaji kazi wa PDPC kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2026.

Kikao hicho kilifanyika tarehe 15 Agosti 2026 katika ofisi za PDPC zilizopo Mtaa wa Moshi, jijini Dodoma.



HABARI PICHA

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia (kushoto) akiwa na wajumbe wa timu ya menejimenti ya PDPC katika Kikao cha Kumi cha Bodi ya Wakurugenzi PDPC kilichofanyika tarehe 15 Agosti 2026 katika ofisi za PDPC zilizopo Mtaa wa Moshi, jijini Dodoma.

HABARI PICHA

Baadhi ya wajumbe wa timu ya menejimenti ya PDPC wakiwa katika Kikao cha Kumi cha Bodi ya Wakurugenzi PDPC kilichofanyika tarehe 15 Agosti 2026 katika ofisi za PDPC zilizopo Mtaa wa Moshi, jijini Dodoma.







MAKALA MAALUM

PDPC Inavyotumia PDPA Kulinda Taarifa Binafsi Za Wananchi Na Kuimarisha Mazingira Ya Uwekezaji Nchini.

Katika uchumi wa kidijitali, taarifa binafsi zimekuwa rasilimali muhimu kwa shughuli za biashara, uwekezaji na utoaji wa huduma. Hata hivyo, thamani yake haiwezi kutenganishwa na wajibu wa kulinda faragha na haki za wananchi. Ulinzi wa taarifa binafsi hujenga uaminifu katika matumizi ya teknolojia, hupunguza hatari za matumizi mabaya ya taarifa na kuchangia mazingira yanayofaa kwa biashara na uwekezaji.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, iliridhia Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 (PDPA), iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2022 na kuwezesha kuanzishwa kwa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) tarehe 1 Mei, 2023. Hatua hizi zimeweka msingi wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na matumizi ya taarifa binafsi katika sekta za umma na binafsi.

Akizindua rasmi PDPC tarehe 3 Aprili 2024, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisisitiza kuwa faragha ni sehemu ya utu na staha ya mwanadamu. Aidha, alielekeza taasisi zote zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi kujisajili na kuzingatia sheria. Maelekezo hayo yalielekeza msisitizo si kwenye teknolojia



pekee, bali pia kwenye uwajibikaji wa taasisi na haki za wananchi katika mazingira ya kidijitali.


Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera na sheria katika eneo hili. Akifunga mafunzo ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) jijini Arusha tarehe 5 Januari 2026, Waziri mwenye dhamana ya Wizara hiyo, Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki (Mb), alisisitiza umuhimu wa taasisi kujisajili PDPC na kuweka mifumo salama ya usimamizi wa taarifa.

Kwa upande wa utekelezaji, PDPC chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia, imeendelea kutoa elimu, kusajili wadhibiti na wachakataji wa taarifa binafsi, kushughulikia malalamiko na kusimamia uzingatiaji wa sheria. Akizungumza kwenye mafunzo ya DPOs jijini Mbeya tarehe 11 Februari 2026, Dkt. Mkilia alionya kuwa ukiukaji wa misingi ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa unahatarisha faragha, usalama na haki za wananchi. Tume pia ilitangaza kuanza kwa ukaguzi wa lazima tarehe 28 Agosti 2026 ili kuimarisha uzingatiaji wa matakwa ya sheria.

Hadi kufikia Oktoba 2026, zaidi ya taasisi 15,000 zilikuwa zimesajiliwa; malalamiko zaidi ya 445 yalikuwa yamepokelewa na kushughulikiwa; na vibali 121 vya usafirishaji wa taarifa binafsi nje ya Tanzania vilikuwa vimetolewa. Hatua hizi zinaonyesha kuimarika kwa taratibu za usimamizi, uwajibikaji na ufuatiliaji wa uchakataji wa taarifa binafsi nchini.

Uhusiano kati ya ulinzi wa taarifa binafsi na uwekezaji unatokana na hitaji la wawekezaji kuwa na uhakika wa usalama wa taarifa, uzingatiaji wa masharti ya kisheria na uwezo wa taasisi kulinda haki za wateja. Uwepo wa mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa unaweza kuongeza imani ya biashara zinazotegemea huduma za kidijitali na kubadilishana taarifa ndani na nje ya nchi. Hivyo, utekelezaji wa PDPA ni sehemu ya mazingira mapana yanayowezesha biashara, ingawa si sababu pekee inayoamua kiwango cha uwekezaji.





Kwa mujibu wa taarifa ya mwenendo wa uwekezaji nchini kwa mwaka 2021–2025 iliyotolewa na Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi (TISEZA) tarehe 7 Januari 2026, miradi iliyosajiliwa iliongezeka kutoka 252 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.7 mwaka 2021 hadi miradi 915 yenye thamani ya dola bilioni 10.95 mwaka 2025. Mwaka 2024, thamani ya uwekezaji iliyotajwa ilifikia dola bilioni 9.3. Takwimu hizi zinaonyesha ukuaji wa uwekezaji katika kipindi ambacho Tanzania pia iliimarisha mifumo yake ya kidijitali na kisheria, ikiwemo ulinzi wa taarifa binafsi.

Ili manufaa ya mfumo huu yaendelee kuonekana, taasisi zinapaswa kujisajili inapohitajika, kuweka hatua za kiufundi na kiutawala za kulinda taarifa, kutoa taarifa kwa uwazi kuhusu matumizi ya taarifa na kushughulikia haki na malalamiko ya wananchi. Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi wana nafasi muhimu katika kuratibu uzingatiaji wa sheria, kutoa ushauri kwa menejimenti na kufuatilia mienendo ya uchakataji wa taarifa ndani ya taasisi.

Wananchi nao wanapaswa kufahamu haki zao na kuwa waangalifu wanapotoa taarifa binafsi, hususani kupitia huduma za mtandaoni. Kwa kushirikiana na wadau, PDPC itaendelea kuimarisha elimu kwa umma, ukaguzi, usimamizi wa malalamiko na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria. Hatua hizi ni muhimu katika kujenga uchumi wa kidijitali unaoaminika, unaolinda utu na faragha ya mwananchi na kusaidia Tanzania kuwa na mazingira salama na yanayotabirika kwa uwekezaji.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

TAARIFA KWA UMMA

KUANZA KWA UKAGUZI WA UZINGATIAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI.

Dodoma – Agosti 28, 2026.

Katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 (PDPA), Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) tayari imeanza zoezi la Ukaguzi wa Uzingatiaji wa matakwa ya Sheria hiyo kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi Nchini.

Tume ilitoa muda wa kutosha kwa taasisi, mashirika, wafanyabiashara na wadau wote wanaokusanya na kuchakata Taarifa Binafsi kujiandaa na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Kwa sasa Tume inaendelea kufanya ukaguzi wa uzingatiaji unaolenga kuhakikisha kwamba Taarifa Binafsi za watumiaji wa huduma mbalimbali Nchini zinakusanywa, kuchakatwa na kuhifadhiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Ukaguzi huu unajumuisha mambo yafuatayo:-

1. Kuhakiki iwapo taasisi inayokusanya na/au kuchakata Taarifa Binafsi imesajiliwa na Tume kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1) na 14(2) vya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44;

2. Kuhakiki usahihi wa Taarifa za usajili zilizowasilishwa na wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi kwenye rejesta ya Tume;

3. Kuhakiki utekelezaji wa majukumu ya Afisa Ulinzi wa Taarifa;

4. Kuhakiki namna Taarifa Binafsi zinavyokusanywa, kuchakatwa, na kuhifadhiwa;

UK.1

Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

TAARIFA KWA UMMA

5. Kuhakiki usalama wa Taarifa Binafsi dhidi ya upotevu, uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa bila idhini kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binasi Sura ya 44;

6. Kuhakiki utaratibu wa usafirishaji wa Taarifa Binafsi nje ya nchi kama inavyoelekezwa kwenye Kifungu cha 31 na Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44; na

7. Kuchukua hatua za kisheria ikiwemo kutoa adhabu na faini kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi wasiozingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44.

Tume inatoa wito kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi kuhakikisha kuwa:-

1. Wamesajiliwa katika rejesta ya Tume;
2. Wanazingatia haki za wahusika wa Taarifa;
3. Wanakusanya na kuchakata Taarifa Binafsi kwa madhumuni halali na mahususi yaliyokusudiwa;
4. Wanawasilisha Ripoti ya Uzingatiaji Kila Robo ya Mwaka;
5. Wanazingatia Sera ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoidhinishwa na Tume;
6. Taarifa binafsi hazisafirishwi nje ya mipaka ya nchi kinyume cha Sheria; na
7. Wanapata ridhaa ya wahusika wa Taarifa kabla ya kukusanya na/au kuchakata Taarifa zao Binafsi, pale inapohitajika.

Tume inautaarifu umma kuwa zoezi la ukaguzi kwa hatua inayofuata litahusisha kutembelea wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi ili kuendelea kujiridhisha na uzingatiaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44. Tume inategemea ushirikiano kutoka kwa wadau wote katika kufanikisha zoezi hili.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti yetu www.pdpc.go.tz au wasiliana nasi kwa namba za simu +255753459155 +25571846253; +255744057652; +255695507751; na barua pepe helpdesk@pdpc.go.tz

Imetolewa na:
Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia
Mkurugenzi Mkuu - PDPC

UK.2

Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.

@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA

CERTIFIED DATA PROTECTION OFFICER PROGRAM

CDPOP

THIRD COHORT: NOVEMBER 2026 (DAR ES SALAAM)

TRAINING DATES:
30TH NOV - 13TH DEC
2026

OFFICIALLY LAUNCHED ON
13TH JULY 2026

Registration 01st October to 29th November 2026

WHO SHOULD ENROL?
DPOs & aspirants
Legal, ICT ,Compliance, Audit, HR, Records Officers and Other field.

WHY ENROL?
Compliance skills
Practical preparation for data protection roles

PROGRAMME STRUCTURE
5 modules
10 credits delivered across five mandatory modules

FINAL AWARD
Certified Data Protection Officer
Awarded upon successful completion

Training Mode: Face to face & Virtual, Exam in person

Why you should enrol

- Understand Tanzania PDPA obligations in practice
- Build privacy policies, records and compliance evidence.
- Handle data subject requests and personal data breaches.
- Conduct DPIAs, audits and regulatory readiness reviews.
- Advise management and build an ethical data culture.

PROGRAM FEE: TZS 2,500,000/=

ENTRY REQUIREMENT
DPOs or aspiring DPOs with a bachelor's degree or diploma in any field.

Programme structure

01 Foundations of Data Protection and Privacy
02 Lawful Processing of Personal Data
03 Rights of Data Subjects and Organisational Responsibilities
04 Governance, Risk Management and Impact Assessment
05 Compliance, Monitoring, Enforcement and Sanctions

FINAL AWARD
Successful learners are awarded the title: Certified Data Protection Officer.

Certified Data Protection Officer Program
Dean contact: Dr Helen Kiunsi | helen.kiunsi@out.ac.tz | +255 715 208 545
Click or Scan to Register



PDPC Yawatahadharisha Wakulima Usalama Wa Taarifa Binafsi Kidigitali

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia amewataka wakulima nchini kuwa makini na matumizi ya Taarifa zao Binafsi hasa wanapotumia mifumo ya kidigitali katika uzalishaji, masoko na shughuli nyingine za kilimo.

Dkt. Mkilia amesema hayo Agosti 08, 2026 wakati akizungumza kwenye kilele cha Maonesho ya Nane Nane - 2026 katika viwanja vya Dkt. John Samuel Malecela jijini Dodoma ambapo amesema Usalama wa Taarifa Binafsi ni muhimu katika kujenga uaminifu kati ya wakulima, wanunuzi, taasisi za fedha, kampuni za teknolojia na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa kilimo.

Maonesho haya ya siku nane (8) yalibebwa na kaulimbiu ya Tambua Soko, Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050 yalifungwa rasmi na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



HABARI PICHA

Baadhi ya watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), wakitoa elimu ya dhana ya Ulinzi wa taarifa Binafsi kwa wananchi waliotembelea Banda la PDPC, kwenye Maonesho ya Nane nane 2026 katika viwanja vya Dkt. John Malecela jijini Dodoma.





HABARI PICHA

Ni baadhi ya Watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ofisi ya Zanzibar wakitoa elimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) kwa wananchi walitotembelea banda la PDPC kwenye maonesho ya Nanenane 2026 yaliyofanyika katika Viwanja vya Dole kwa upande wa Visiwani Zanzibar.





Huduma kwa wateja:

Simu:

+255753459155
+255718462536
+255744057652
+255615779070
+255736110505

Barua pepe:

helpdesk@pdpc.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi,
S.L.P 1105, 1 Mtaa wa Moshi,
Viwandani, 41102 Dodoma.